Mwanadamu na Asili yake

"Mwanamume na mwanamke waliumbwa wakiwa na sura ya Mungu binafsi wakiwa na uwezo na uhuru wa kufikiri na kutenda. Japo waliumbwa huru, kila mtu katika umoja wote wa mwili, akili na roho, walimtegemea Mungu kwa uhai, kuvuta pumzi na mengineyo yote. Wakati wazazi wetu walipomkaidi Mungu, sura ya mwumbaji iliharibiwa na wakawa watu wa kufa. Uzao wao hushiriki hali hii ya mwanadamu aliyeanguka na matokeo yake yote. Huzaliwa wakiwa na unyonge na kuelekea kutenda dhambi. Lakini Mungu katika Kristo, aliupatanisha ulimwengu kwa nafsi yake na kwa roho yake akarejeza kwa watu wenye hali ya kufa taswira ya Mwumbaji. Walioumbwa kwa utukufu wa Mungu, wameitwa kumpenda Yeye, kupendana wao kwa wao na kutunza mazingira." (Mw. 1:26,27, 2:7, Zab.8: 4- 8, Mdo. 17:24-28, Mw. 3:4, 6-9, 15 -19, 24 Zab. 51:5, Rum 5:12-17, 2 Cor. 5:19,, 20, Zab. 50:10, 1 Yoh. 4:7, 8) Kanuni za Kanisa, Msingi wa Imani no. 7)

Asili ya Mwanadamu

Wazo la kumuumba mwanadamu lilitoka kwa Mungu. (Mwa. 1:26.) Na wakati anamuumba, alitekeleza wazo lake kwa kuumba watu wawili, mtu mume na mtu mke, akawaita jina lao Adamu. (Mw. 1:27; 5:1, 2.)

Mwanadamu aliumbwa kwa udongo na pumzi (Mw. 2:7) Vitu viwili vilitengeneza mtu, udongo na pumzi ya uhai. Kilichopatikana kutokana na mwunganiko wa udongo na pumzi kimeitwa nafsi hai, yaani kama tungekuwa tunafanya hesabu, udongo + pumzi ya uhai = nafsi hai. Nafsi hai haiwezi kuwa nafsi hai ikiwa kimojawapo kati ya udongo au pumzi ya uhai kitaondolewa. Kwa hiyo, nafsi hai ni kitu kisichoweza kugawanyika ili kila kipande kibaki na maisha yake)yanayojitegemea peke yake. (cf. Mhu. 12:7)

Aliumbwa kwa sura ya Mungu (Mwa.1:26) Viumbe vingine vilikuwa kwa jinsi zake (Mwa.1:2, 24, 25). Lakini mwanadamu alikuwa kwa mfano wa Mungu. Na Luka anasema, Adamu ni mwana wa Mungu (Luk.3:38)

Mwanadamu ana hadhi ya juu. Aliumbwa akiwa na hadhi ndogo kuliko malaika lakini alipewa kusimamia uumbaji wa Mungu. (Mwa. 1:28; Zab. 8:4-9)

Umoja wa wanadamu. Wote tulianzia kwa Adamu. Mungu alifanya kila taifa la wanadamu kutoka mmoja (Mdo.17:26). Kwa kosa la Adamu wote tumeanguka dhambini na kwa tendo la Yesu, wote twaweza kuokolewa (Rum.5:12, 19; 1Kor.15:21, 22)

Umoja wa Asili ya Mwanadamu (Mwa.2:7)

Udongo**:** Tafsiri ya udongo haina shida. Ni sehemu ya ardhi.

Pumzi ya Uhai. (Mwa.2:7). Wakati Mungu alipobadili maada ya dunia kuwa kiumbe hai, alipulizia pumzi ya uhai. Alipulizia pumzi ya uhai, pumzi za Mwenyezi (Ayu.33:4), cheche ya uhai.

Mwanadamu - Nafsi Hai . Hesabu ya Maandiko iko wazi. Udongo jumlisha pumzi ya Mungu ni sawa na nafsi hai. Siyo wanadamu pekee waliopewa pumzi ya uhai. Nafsi hai hujumuisha

pia wanyama wa baharini, vitambaavyo, na wanyama (Mwa.1:20, 24; 2:19). Siyo kwamba mwanadamu akapokea roho, bali akawa nafsi (roho) hai.

Umoja usiogawanyika- Mwanadamu ni kiumbe kimoja kisichogawanyika. Je, kuna uhusiano gani baina ya nafsi na roho?

1. Maana ya Biblia ya Nafsi.

Katika Agano la Kale, neno la kiebrania lililotafsiriwa nafsi ni *nephesh*. Ndivyo Mw. 2:7 inavyosema mtu akawa nafsi hai. Kwa jinsi hiyo hiyo kila mtoto mchanga anapozaliwa, nafsi hai huongezeka. Kwa hiyo, nephesh siyo sehemu ya mwanadamu hai bali ni mwanadamu mzima. Anavyokufa binadamu vivyo hivyo na mnyama (Mwa.7:20–23) Wakati wa Nuhu vilikufa viumbe vyote isipokuwa Nuhu na waliobaki ndani ya safina. Kwa kuwa roho (nephesh) ndiyo nafsi hai, roho nayo inakufa (Ez.18: 4).

Katika Agano Jipya lililoandikwa Kigiriki, neno litumikalo kwa nafsi ni *psuche*. Hutumika kwa wanadamu na wanyama (Uf. 16:3) “Na huyo wa pili akakimimina kitasa chake juu ya bahari, ikawa damu, kama damu ya mfu, na vitu vyote vyenye roho ya uhai katika bahari vikafa.” Kwingine roho ina maana ya uhai (Mat. 2:20, 6:25, 16:25). Kwingine roho inamaanisha watu (Mdo. 7:14, 27:37, Rum. 13:1 1Pet.3:20) Hutumika kwa nafsi (Mt. 12:17. 2 Kor.12:15) Na kwingine humaanisha hisia (Mk.14:34 Luk. 2:35) au akili (nia) (Mdo 14:2, Filipi 1:27) au moyo (Ef. 6:6)

Katika yote haya, lengo ni kuhitimisha kwamba psuche (roho) haina hali ya kutokufa bali ina hali ya kufa. (Uf. 16:3)

2. Maana ya Pumzi ya Uhai

Neno *ruach* lililotafsiriwa pumzi, hupatikana kwenye Agano la Kale mara 377. Kufuatana na Ayubu 33:4, ni pumzi ya Mungu inayotia uhai, Inaitwa upepo, roho au pumzi (Mw. 8:1) Na kila chenye uhai, Hutumika kuonyesha hali ya kuwa mzima wenye nguvu (Amu. 15:19). Hutumika wakati mwingine kuonyesha ujasiri (Yosh. 2:11) hasira au kukosa uvumilivu (Amuz. 8:3). Pia huonyesha hadhi (Isa. 54:6), tabia adilifu (Ez. 11:19) “Nami nitawapa moyo mmoja, nami nitatia roho mpya ndani yao; nami nitauondoa moyo wa kijiwe katika miili yao, name nitawapa moyo wa nyama.”

Kwa maana ya upepo au pumzi, hakuna tofauti kati ya binadamu na mnyama kwenye kifo (Mh. 3:19 -21). Roho humtoka mwanadamu akifa Zab. 146:4 na humrudia Mungu Mh. 12:7 (Angalia pia Ay. 34:14). *Ruach* hutumika mara nyingi kumaanisha Roho ya Mungu (Isa. 63:10). Hakuna kwenye Agano la Kale ambako roho (*ruach*) imepata kuishi kwa kujitegemea nje ya mwili.

Katika Agano jipya, neno lililo na maana ya *ruach* (Kiebrania) ya agano la kale ni *pneuma* (Kigiriki) – kupuliza, kupumua. Kama ilivyo kwa ruach, hakuna chochote ndani ya mwanadamu chenye kuweza kuishi nje ya mwili.

Roho/Moyo (pneuma) imetumika pia kuonyesha mtizamo – (Rum. 8:15, 1 Kor 4:21, 2 Rum. 1:7, 1Yoh.4:6) na hali mbali mbali za kibinadamu kama katika (Gal. 6:1, na Rum. 12:11). Pneuma hutoka mtu anapokufa (Luk. 23:46, Mdo. 7:59). Kama ruach, pneuma pia inatumika tunaposema Roho ya Mungu (1Kor.2:11, 14, Ef.4:30, Ebr.2:4 1Pet.1:12, 2Pet. 1:21).

3. Muungano wa mwili, moyo na roho

a) ***Muungano wa viwili*.** Biblia haisemi uhusiano uliopo baina ya mwili, moyo na roho. Wakati mwingine nafsi na roho hutumika kwa kubadilishana "moyo wangu wamwadhimisha Bwana, roho yangu imemfurahia" (Luk. 1: 46, 47). Mara moja, Yesu amemsema mwanadamu kuwa ni mwili na roho (Mt.10:28). Mahali pengine, Paulo anamwona binadamu kuwa ni mwili na roho (1Kor.7:34)

b) ***Muungano wa vitatu.*** Paulo ambaye alipata kumzungumza mwanadamu kuwa wa muungano wa viwili, amesema kwenye 1Thes.5:23 kuwa mwanadamu ana nafsi, roho na mwili. Hapa, roho yaweza kuwa kanuni ya juu ya akili inayowasiliana na Mungu (Rum. 8:16). Kufanywa upya nia, hutubadilisha (Rum.12:1, 2)

c) ***Muungano usiogawanyika.*** Mwili, moyo na roho hutenda kazi kwa kushirikiana ikionesha hali ya mtu kiroho, kiakili na kimwili.

Mwanadamu katika Sura ya Mungu (Mwa.1:27 Ina maana gani?)

Aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Malaika ambao kama Mungu ni Roho (Yoh.4:24; Ebr.1:7, 14). Lakini huonekana katika umbo la kibinadamu (Mwa.18:1-19:22; Dan. 9:21; Luk.1:11-38; Mdo.12:5-10). Je, roho yaweza kuwa na mwili wa kiroho? (cf. 1Kor.15:44). Biblia inasema Musa, Haruni, Nadabu, Abihu na wazee sabini waliona sehemu ya mwili wa Mungu (Kut.24:9-11; Kut.33:20-23). Danieli alimwona Mzee wa Siku akihukumu (Dan.7:9, 10). Kristo anaelezewa kuwa ni mfano wa (taswira ya) Mungu asiyeonekana (Kol.1:15) na chapa ya nafsi ya Mungu (Ebr.1:3). Maelezo yanaelekea kupendekeza kuwa Mungu ni nafsi yenye umbo. Mwanadamu aliumbwa kwa hadhi ndogo kuliko malaika (Ebr.2:7) yamaanisha alikuwa na hali ya kiroho na kiakili. Alikuwa mkamilifu (Mh.7:29) akiwa mwenye haki na mtakatifu (cf.Efe.4:24) na alikuwa sehemu ya uumbaji ambayo Mungu aliitamka ni njema sana (Mwa.1:31). Alikuwa na uhuru wa kuonyesha upendo ulio tabia ya Mungu (1Yoh.4:8) akilenga kufikia upendo kwa Mungu kwa moyo wote, roho yote na nguvu zote na upendo kwa wengine kama nafsi yake (Mt.22:36-40).

Aliumbwa ahusiane na watu wengine. Siyo vema mtu huyu awe peke yake (Mwa.2:18) na hivyo kuna mahusiano yanaoingia kutokana na familia, jamii na hata taifa. (Mdo.17:26)

Aliumbwa Kuwa Wakili wa Mazingira. Akiwa mtawala wa ndege wa angani, wanyama na nchi (Mwa.1:26) ni wakili kwa niaba ya Mungu. Daudi alisema, Mungu alimtawaza juu ya kazi zake (Zab.8:4-9).

Aliumbwa kumfuata Mungu. Japokuwa ni wanadamu, tumeitwa kumwiga Mungu. Amri ya nne, inasema tumwige Mungu kufanya kazi sita, na sabato tupumzike (Kut.20:8-11).

Aliumbwa akiwa na hali ya kutokufa yenye sharti. Hali ya mwanadamu ya kutokufa ilitegemea utii wake kwa amri ya Mungu (Mwa.2:16, 17) na alipokosea, hakuweza kuwa na hali hiyo tena (Mwa.3:19, 22, 24).

Kuanguka dhambini

***Asili ya Dhambi*:** Ikiwa Mungu aliumba kitu chema (Mwa.1:31), dhambi ingeweza kuanzia wapi?

1. Mungu na Asili ya Dhambi.Biblia husonda kwamba Mungu ni Mtakatifu (Isa.6:3). Hakuna ukengeufu ndani yake kwani "kazi yake ni kamilifu, njia zake zote ni haki, ni wa uaminifu asiye na uovu" (Kumb.32:4). Mungu asidhaniwe kutenda udhalimu wala uovu (Ayu.34:10). Haiwezekani kumjaribu Mungu kwa maovu, wala yeye hamjaribu mtu (Yak.1:13). Mungu huchukia dhambi (Zab.5:4; 11:5). Uumbaji wa Mungu kwa asili ulikuwa mwema (Mwa.1:31). Badala ya kuwa chanzo cha dhambi, yeye ni chanzo cha wokovu kwa hao wanaomtii (Ebr.5:9).

2. Mwanzilishi wa Dhambi. Mungu angeliweza kuzuia dhambi kama angeumba roboti, yaani viumbe visivyo na uhuru wa kuamua. Kwa kuumba viumbe huru ina maana alikabiliwa na hatari ya maamuzi yaliyo kinyume na mapenzi yake. Bahati mbaya Lusifa, malaika wa ngazi ya juu aliingiwa kiburi (Eze.28:17; cf 1Tim.3:6). Kwa kutokuridhika na nafasi yake (Yud. 6) , alianza kutamani nafasi ya Mungu (Isa.14:12-14). Kwa kutamani kushika nafasi ya Mungu, malaika huyu alianza kupanda mbegu za kutokuridhika na akapata wafuasi. Vita ikatokea, (sasa malaika huyu anaitwa) Shetani akafukuzwa mbinguni yeye pamoja na malaika wenzake. (Ufu.12:4, 9-12).

3. Asili ya dhambi kwa Mwanadamu. Pasipo kuzuiwa na kufukuzwa kwake mbinguni, Shetani alitaka wengine pia wamwasi Mungu. Aliingia katika bustani ya Edeni akiwa na umbo la nyoka na akamshawishi Hawa kula matunda ya mti uliokatazwa. (Mwa.3:4, 5) Hawa alishawishika akala, akampelekea na mumewe naye akala. (Mwa.3:6). Hivyo dhambi ikaangia duniani (Rum.5:12)

Athari za Dhambi

1. Athari za haraka. Kufumbuliwa macho kuliwafanya Adamu na Hawa waone aibu (Mwa.3:7). Badala ya kufanana na Mungu kama walivyoahidiwa na Shetani, waliogopa wakajaribu kujificha (Mwa.3:7-8). Mahusiano ya ndoa yaliharibika kwa Adamu kulaumu uwepo wa Hawa (Mwa.3:12) na Hawa kulaumu uwepo wa nyoka (Mwa.3:13). Matamshi ya laana, yalifanya nyoka atembee kwa tumbo (Mwa.3:14), mwanamke kuzaa kwa uchungu na kutawaliwa na mwanaume (Mwa.3:16), kulaaniwa ardhi, kuwepo miimba na michongoma na kazi za jasho (Mwa.3:17-19). Kusisitiza kuwa sheria yake haibadiliki, Mungu alisema "kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi". (Mwa.3:19). Alitekeleza hukumu yake kwa kukata mawasiliano ya moja kwa moja (Mwa.3:8), kuwafukuza watoke Edeni na kuwazuilia wasile matunda ya mti wa uzima (Mwa.3:23, 24). Hivyo, Adamu na Hawa na uzao wao wakawa watu wa kufa. (Mwa.3:22)

2. Tabia ya dhambi. Maelezo mengi ya Maandiko Matakatifu, hueleza kuwa dhambi ni uovu, pale viumbe huru wanapochagua kutenda kinyume na mapenzi ya Mungu (Mwa.3:1-6; Rum.1:18-22)

a) Maana ya dhambi. Maana ya kibiblia ya dhambi inajumuisha uasi (1Yoh.3:4), mtu kushindwa kutenda vema wakati anajua (Yak.4:17) na kutokufanya matendo kwa imani

(Rum.14:23). Dhambi haina kutokuhusika na upande wowote “asiye nami yu kinyume changu” (Mt. 12:30). Kutokumwamini ni dhambi (Yoh.16:9). Dhambi ni dhambi, kwamba ni amri moja imevunjwa au nyingi (Yak.2:10).

b) Dhambi huhusisha mawazo na matendo. Mara nyingi dhambi husemwa kuhusu matendo. Lakini Kristo alisema dhambi huhusisha mawazo pia. (Kut.20:13 cf. Mt.5:21, 22; Kut.20:14 cf Mt. 5:27, 28)

c) Dhambi na hatia. Dhambi huleta hatia na hatia huleta hukumu (Rum.3:19). Isipothibitiwa, itaharibu, mwili, akili, moyo na roho. Hatimaye italeta mauti. (Rum.6:23). Kinachoharibu dhambi ni msamaha (Mt.6:12). Kwa waliolemewa na mzigo wa dhambi Yesu amealika wakapumzike kwake. (Mt.11:28).

d) Kinachothibiti dhambi. Dhambi huwa ndani ya kinachoitwa na Biblia moyo, au kama tujuavyo, ni nia. Kutoka moyoni, huchipua mambo ya uzima (Mith.4:23). Ni mawazo ya mtu ndiyo hutia unajisi (Mt.15:19). Ni kwa moyo, mtu mzima huvutiwa kutenda maovu (Yer.17:9).

1. Athari za dhambi kwa Mwanadamu. Athari za dhambi ya Adamu na Hawa kwa mwanadamu zilikuwa kubwa. Mwana wao wa kwanza aliua. Uzao wao mara moja ulidharau ndoa na kuanza mitala, na haikuchukua muda mrefu dunia ikajaa dhuluma (Mwa.4:8, 23; 6:1-5, 11-13).

a) ***Hali ya dhambi kwa wanadamu wote.*** Uzao wa Adamu huchangia asili ya dhambi ya Adamu (Mwa.5:1, 2). Daudi anasema hakuna aliye hai mwenye haki (Zab.143:2; cf 14:3). Hakuna asiyetenda dhambi (1Fal.8:46). Nani awezaye kusema mie ni msafi (Mith.20:9; Mh. 7:20). Agano jipya nalo lasema wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu (Rum.3:23). Tukisema hatuna dhambi, twajidanganya (1Yoh.1:8).

b) ***Hali ya dhambi hurithiwa au humkuta mtu baadaye?*** Katika Adamu wote wanakufa (1Kor.15:22). Kwa dhambi ya mtu moja, wote dhambi iliingia duniani, ikaleta mauti kwa kuwa wote wametenda dhambi (Rum.5:12). Hakuna awezaye kutoa kitu safi kutoka katika uchafu (Ayu.14:4). Daudi asema alizaliwa kwenye dhambi…(Zab.51:5). Nia ya mwili ni uadui dhidi ya Mungu… wasio wa Mungu hawawezi kumpendeza (Rum.8:7, 8). Kabla ya kuongoka, ni wana wa ghadhabu (Efe.2:3).

c) ***Kuondosha tabia ya dhambi.*** Hakuna juhudi binafsi itakayoondoa dhambi (Yer.13:23; Yoh.15:5). Atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi. Yesu ametuhakikishia akituweka huru, tutakuwa huru kweli kweli. (Yoh.8:36). Twaweza kutenda mema tukikaa ndani yake (Yoh.15:4, 5). Hata mtume Paulo alisema hawezi kutenda jema, akajililia nani atamwokoa na mwili wa mauti? (Rum.7:15, 19, 20, 22-24). Paulo hatimaye anakiri nguvu ya kimbingu inahitajika kukomesha dhambi (Rum.7:25; 8:1). Nguvu ya kushinda dhambi ni karama ya Mungu inayobadilisha. (Efe.2:1, 3, 8-10). Kuzaliwa kiroho hubadili maisha (Yoh.1:13; Yoh.3:5) kiasi kwamba twaweza kusema juu ha kuzaliwa upya (2Kor.5:17). Kuwa kiumbe kipya hata hivyo hakuondoi uwezekano wa kufanya dhambi (1Yoh.2:1).

4. Uibukaji na anguko la Mwanadamu. Tangu uumbaji Shetaji amejitahidi kuhafifisha imani ya wanadamu kwenye Maandiko Matakatifu. Wakristo wengi waliipokea nadharia ya uibukaji na kuiingiza kwenye mafundisho.

a) ***Mtazamo wa Biblia wa mwanadamu na uibukaji.*** Biblia inakataa tafsiri inayofanya kitabu cha Mwanzo kuwa mifano au vielelezo wa hali nyingine. Waandishi wa Biblia wenyewe hutafsiri Mwanzo 1 – 11 kuwa historia ya kawaida. Adamu, Hawa, Nyoka na Shetani wanaonekana kuwa wahusika katika pambano kuu. (Ayu.31:33; Mh.7:29; Mt.19:4, 5; Yoh.8:44; Rum.5:12, 18, 19; 2Kor.11:3; 1Tim.2:14; Ufu.12:9).

b) Kalvari na Uibukaji. Kalvari hupinga uibukaji. Ikiwa hapakuwa na anguko, kwa nini Yesu ahitajike kufa kwa ajili ya mwanadamu?

c) Kufanyika Mwili na Uibukaji. Ikiwa Mungu aliweza kufanya muujiza wa kumfanya Yesu afanyike mwili, angeshindwaje kumfanya Adam katika ile nafasi ya kwanza?

d) Je, Mwanadamu amekuwa wa miaka mingi? Iko imani kwamba mwanadamu akipewa wakati wa kutosha, ataondokana na matatizo yake. Hata hivyo, kwa kile kinachoitwa maendeleo ya kisayansi, dunia imekuwa eneo hatari kuliko wakati uliopita. Hivyo mwanadamu anahitaji mwokozi nje ya uanadamu ili aokolewe.

Miali ya Matumaini. Kupungukiwa mwanadamu ni kukubwa hata walimsulubisha mwumbaji wao. Maneno ya mwanadamu kuwa chini ya malaika bali ametawazwa juu ya kazi za mikono ya Mungu ni ya kweli kabisa. (Zab.8;5, 6 cf. Ebr.2:7). Pamoja na anguko bado hadhi ya uanadamu iko juu. Daudi alishangalia, Ee Mungu, jinsi lilivyo tukufu jina lako. (Zab.8:9)

Agano la Neema

Baada ya kutenda dhambi, Adamu na Hawa walikuwa wadhambi, wasioweza kumpinga Shetani. Je, wangeweza kuwa huru au waliachwa wapotee?

Agano lilitolewa wakati wa Anguko. Kabla Mungu hajatamka adhabu kwa Adamu na Hawa, aliwapa matumaini kwa kutangaza agano la neema. “nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wake na uzao wako; huo utakuponda kinywa, na wewe utamponda kisigino”. (Mwa.3:15). Wanaokubali neema ya Mungu wataujua uadui na kwa imani watashiriki ushindi wa Kristo Kalvari.

Agano Lilianzishwa Kabla ya Uumbaji. Agano la neema halikuanzishwa baada ya mwanadamu kuanguka. Alituchagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu ili tuwe watakatifu…wanawe kwa njia ya Yesu Kristo. (Efe.1:4-6; 2Tim.9). Kujitoa Yesu kulijulikana kabla ya misingi ya ulimwengu. (1Pet.1:20). Agano lilijengwa kwenye ahadi na kiapo cha Mungu mwenyewe (Ebr.6:18). Yesu alikuwa amana ya agano (Ebr.7:22). Si malaika au mwanadamu, angeweza kutimiza madai ya sheria ya Mungu iliyovunjwa, isipokuwa Yesu (Rum.5:12-21; 1Kor.15:22).

Yesu siyo tu amana, bali pia mtendaji wa agano. Alikuja kutenda mapenzi ya Baba yake (Yoh.6:38 cf.5:30, 43). Mapenzi ya Baba ni amwaminiye Mwana apate uzima wa milele (Yoh.6:40). Uzima wa milele ni kumjua Baba na Yesu (Yoh.17:3).

Mwisho wa huduma ya Yesu duniani alisema, nimeimaliza kazi (Yoh.17:4). Msalabani Yesu alipaza sauti akisema, “Imekwisha”.
(Yoh.19:30).

Agano Kufanywa Upya. Wanadamu walikataa agano kabla na baada ya gharika (Mwa.6:1-8;
11:1-9). Mungu alipotoa agano tena, alililifanya na Ibrahimu (Mwa.2218 cf. 12:3; 18:18). Ibrahimu alikuwa mwaminifu kwa masharti ya agano (Mwa.15:6). Pamoja na kujengwa kwenye neema, agano pia liliegemea kuitambua sheria ya Mungu (Mwa.17:1; 26:5). Imani ya Ibrahimu ilikuwa makini hadi akaitwa baba wa imani (Rum.4:11). Ni kielelezo cha haki kwa imani (Rum.4:2, 3; Yak.2:23, 24). Baraka inaenda kwa uzao wa Ibrahimu wenye imani sawa naye (Gal.3:7). Kila mtu duniani aweza kuokolewa kwa sharti la kuwa ndani ya Kristo, na kuwa uzao wa Ibrahimu (Gal.3:29). Kwa mtazamo wa Mungu, agano la Sinai vilevile lilikuwa agano la neema kwa Ibrahimu lililofanywa upya (Ebr.9:1). Lakini Waisraeli walipotosha kuwa agano la matendo (Gal.4:22-31).

Agano Jipya. Baadaye sehemu ya Maandiko huzungumzia agano jipya lililo bora zaidi. Halifanyi hivyo kwa sababu agano la milele lilibadilishwa, ila (1) kutokana na Waisraeli kutokuwa waaminifu, agano la milele limepotoshwa na kuwa mfumo wa matendo. (2) liliambatana na ufunuo mpya wa upendo wa Mungu kupitia Yesu Kristo na (3) halikutimia hadi lilipokamilishwa msalabani kwa damu ya Kristo. (Dan.9:27; Luk.22:20; Rum.15:8; Ebr.9:11-12). Agano hili lafanya mtu kuzaliwa upya, na kuwezesha utii wa amri za Mungu kutoka moyoni (Yer.31:33). Hiyo ndiyo haki ya Kristo inayofanya mtu kuzaa matunda ya roho, upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili uaminifu, upole, kiasi (Gal.5:22, 23)